



Tahadhari wakati unapotumia mawe madini

Kondoo wakikula kiasi kikubwa cha mawe madini wakati mmoja watapata madhara ya sumu ya Urea. Ni muhimu wanyama watangulizwe kwa mawe pole pole na mseto usiwe laini sana ndio wanyama wasikule kuzidi kiasi.

Kuning'iniza mawe hayo badala ya kuyaweka mahali paliponyooka huwazuia wanyama kuuma haya mawe.

Kuwapatia wanyama mawe hayo

Mawe ya madini yana ladha nzuri na sharti yawekwe yakiwa yameinuliwa ili kufanya wanyama warambe badala ya kutafuna.

Mawe yenye dawa husaidia sana kukabiliana na maambukizi mapya ya minyoo. Inapendekezwa kwamba mifugo wapewe dawa za minyoo kabla ya kuwapatia mawe madini.



Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P. 57811, NAIROBI.
Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344
Baruapepe: resource.centre@kari.org
Tovuti: www.kari.org

Watayarishaji:

Mugambi, J.M. Nginyi J.M. na Rugutt, M.K.

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

Mkurugenzi wa Kituo,

KARI-Muguga North
S.L.P. 32 Kikuyu 00902
Simu: 066 32106/7, 32000
Nukulishi: 32450
Baruapepe: vrckari@yahoo.com

Vijitabu vya KARI vya taarifa nambari / 25 / 2008

Shilingi 20 za Kenya

Jinsi ya kutayarisha mawe madini ya kuua minyoo ya mifugo na kuongeza madini



Utangulizi

Mawe madini yenye dawa ni nini?

Mawe ya madini yenye dawa ni chakula chenye nguvu nyingi na pia nyongeza ya madini yaliyo na madawa ya kuangamiza minyoo.

Yanatengenezwa kutokana na asilia zinazopatikana kwa urahisi. Mawe hayo hayapatikani katika soko la biashara Kenya lakini teknolojia ya kuyatengeneza inapatikana kwa urahisi.

Faida ya mawe yenye chakula na dawa

Mawe ya chakula na dawa hupatia nyongeza ya nitrojeni, madini na nishati kwa wanyama. Hii ni muhimu sana hasa wakati wa upungufu wa lishe ya mifugo kwa muda mrefu kama ilivyo kawaida kati sehemu kavu na zilizo kavu kiasi nchini Kenya. Kutumia mawe hayo yenye dawa huwasaidia wanyama kupitisha kipindi hiki cha upungufu kwa kupunguza athari za magonjwa au maambukizi.

Katika maeneo yaliyo na mvua nyingi, matumizi ya mawe haya hukinga minyoo kuambukiza mifugo upya. Hii inapunguza kutegemea dawa za minyoo kila wakati. Mawe haya hupunguza athari mbaya zinazoweza kuhusishwa na matumizi mengi ya madawa.

Vitu vya kutengeneza mawe dawa

Molasi

Mbolea ya 'Urea'

Mseto wa madini

Makapi ya mahindi (au kiungo cha kuongeza kiwango)

Simiti

Chumvi ya mezani.

Dawa ya minyoo* (dawa ya mawe yenye madawa)

Maji.

* Kipimo cha ng'ombe wa kilo 100 ya benzimidazole anthelimitiki kwa kila kilo moja ya mseto wa dawa. Dawa inayopendekezwa sana ni Zerofen na Panacur.

Jinsi ya kutengeneza mawe ya madawa

Njia ya kutengeneza mawe ya dawa ni kama ile ya kutengeneza mawe ya simiti.

Viungo sharti vichanganywe vizuri, kwa kutumia mashine ya kuchanganya simiti au chombo kingine kama hicho. Hatua za kutengeneza mawe 20 ya kilo 5 ni kama zifuatazo.

Hatua ya kwanza

Tia maji lita 5 kwenye mtambo wa kuchanganya simiti. Ongeza kilo 10 za mbolea ya 'urea' kwenye mtambo wa kuchanganya. Zungusha mtambo hadi mseto huo uwe mwafaka.

Hatua ya pili

Ongeza lita moja ya dawa ya anthelmintic (Asilimia 10 ya dawa inayofaa kama vile Zerofen au Panacur).

Hatua ya tatu

Pima kilo 12 za simiti na uchanganye polepole na maji lita 3 hadi mchanganyiko laini upatikane.

Mwaga mchanganyiko huu katika mtambo unaozunguka na uongeze kilo tatu za chumvi ya kawaida na kilo 5 za madini mseto.

Hatua ya nne

Pima kilo 25 za molasi na uweke kwenye mtambo unaozunguka. Tumia maji moto lita 2 kusafisha vihifadhio vya simiti na molasi na uongeze katika mtambo.

Hatua ya tano

Pima kilo 35 za makapi ya mahindi na uziweke katika ule mtambo wa kuchanganya simiti. Zungusha mtambo mpaka rojo rojo yote ifanane.

Rojorojo inayopatikana ni mwafaka kuumba miundo yoyote na viwango tofauti zinzohitajika.

Hatua ya sita

Paka upande wa ndani wa vihifadhio mafuta ili iwe ni rahisi kuziondoa baada ya kukomaa. Mafuta yoyote ya nyumbani yanaweza kutumika, kwa madhumunii haya.

Mwaga rojorojo ile kwenye bakuri 20 za uzani wa kilo 5 kila moja. Mawe hayo yaachwe yakauke kwenye jua kwa takriban masaa mawili.

Baadaye, mawe yaondolewe kutoka kwa bakuri hizo na yaendeleo kukaukia ndani ya nyumba kwa kipindi cha juma moja hadi mbili kutegemea hali ya anga.